Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili A: literature – Standard level – Paper 1
# Swahili A : littérature – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili A: literatura – Nivel medio – Prueba 1

Wednesday 10 May 2017 (afternoon)
Mercredi 10 mai 2017 (après-midi)
Miércoles 10 de mayo de 2017 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

**Instructions to candidates**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a guided literary analysis on one passage only. In your answer you must address both of the guiding questions provided.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

**Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez une analyse littéraire dirigée d'un seul des passages. Les deux questions d'orientation fournies doivent être traitées dans votre réponse.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[20 points]**.

**Instrucciones para los alumnos**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un análisis literario guiado sobre un solo pasaje. Debe abordar las dos preguntas de orientación en su respuesta.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.

2217 – 0199



© International Baccalaureate Organization 2017

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hivi. Ni lazima kuzingatia maswali mawili uliyotolewa kama mwongozo kwenye jibu lako.

**1.**

Uchaguzi ulipokaribia, Zena aliamua kuwaelezea wazazi wake nia yake. Siku moja baada ya chakula cha mchana, Zena aliwapasulia mbarika. Mamake, mdomo ulimfunguka lakini hakuwa na la kusema. Babake naye alitulia tulii kama maji ya mtungini. Baada ya muda, kama kwamba sasa wamepotokwa, mamake akaanza kusema.

"He! Hiyo kasheshe, huu ndio mwaka wa kuvuliwa nguo. Mtoto we! Hujatosheka? Umeona sasa hutajwi tena midomoni unataka uanzwe tena kutafunwa kama ubani?"

"Mama nawe, wewe unafikiria yale watu watakayosema tu hufikirii kuhusu suala lenyewe. Unaonaje ni vizuri au si vizuri?" Zena akamjibu.

Mamake akajibisha kwa sauti, "Si-semeje kuwa swala ni zuri au si zuri na tayari nakueleza kuwa wataka tusemwe? Hilo tayari ni jawabu kuwa sikuyapendelea hata kidogo."

"Baba nawe je waonaje? Tumuache mama na mawazo yake?" Zena akamgeukia babake na kumuuliza.

Mzee Saidi alinyamaza kwa muda kama hakusikia lililoulizwa mpaka Zena akaona labda babake hakusikia. Mzee Saidi alionekana kama yu mbali kimawazo. Lakini kama wasemavyo kimya kina mshindo mkuu. Alipofungua mdomo alionekana ameyawaza kwa kina. "Mamangu hilo ni gumu!" Alinyamaza tena kwa muda na Mzee Saidi alipotopokwa alimuuliza Zena tena, "Mwanangu umelifikiria hili?" Zena naye akajibu, "Ndiyo baba kwa makini sana."

"Una hakika?" aliuliza tena mzee Saidi.

"Baba limenichukua siku nyingi hata nilipoamua," Zena akajibu.

"Basi, kama umefikiri na ni uamuzi wako, ndilo ninalotaka kujua. Maana ulipoachwa na Ali nilikuuliza vivyo na ukawa umeamua na sasa kama umeamua sawa," babake akamwambia kisha akaendelea, "Maana sitaki kukulazimisha na jambo. Mtu mwanaharamu huzaa mara moja mara ya pili huambiwa ni kusudi. Bado nakumbuka nilivyokukosea. Uliposema wataka kuendelea na masomo, nikasema hakuna haja kwa vile kulikuwa na mume ambaye tayari amesimama akitaka kukuoa. Lakini nakiri kosa langu na uliteseka sana mwanangu. Naomba unisamehe, na wakati ule ulipotaka kuachwa ukikumbuka nilikuuliza vile vile kama sasa. Na kama umefikiria basi mwanangu. Lekea kwa mola wako uombe Mungu nami niko nawe mia fil mia."

Zena aliyakumbuka hayo maneno ya babake na akasikia roho yake ikijawa na huruma kwa babake. Alikumbuka matusi yaliyotolewa, na babake hakuyajali wala kujibisha. Mzee Saidi siku zote alikuwa na msemo wake usemao "muungwana akivuliwa nguo hutama hainuki kusimama." Nao walionyesha uungwana wao na sasa alijua itabidi wafanye vivyo tena.

Siku zilisonga mbele sasa ikabakia mwezi tu hadi uchaguzi. Zena hakuwa na wasimamizi wengi kama vile hakuwa na pesa za kulisha. Ni watu wa aila yake na marafiki wachache waliomuunga mkono. Hili halikumfisha moyo. Zena alitayarisha mabango yake ya rangi nyeusi na nyeupe kwa vile vijipesa vyake havikutosha hata kufanya ya rangi. Mikutano ya hadhara ikaanza kuitishwa.

Wafuasi wake wengi wakiwa ni nduguze, binamu na jamaa zake wengine; hawakukosea waliosema damu nzito kuliko maji. Akapata mashababu waliobandika mabango yake. Lakini ikawa ni kazi ya bure. Asubuhi ya siku ya pili kukiamkiwa mabango yote ya Zena yamejazwa rangi na mengine yameandikwa matukano ya mbwa kasoro mkia.

Lililomshangaza Zena ni kusikia wanawake wenyewe wenziwe wakimtafuna kama chingamu. Yeye amejitolea kwa hali na mali kujaribu kunyanyua hali zao na hali wenyewe hata hawanayo. Kwa vile alikuwa anataka kupata kura za wanawake ilibidi awe akihudhuria harusi zote na matanga ijapokuwa hakuyapendelea mambo hayo.

Siku moja aliingia katika nyumba mojawapo iliyokuwa na tausia jioni, basi alipoingia alisikia wanawake wengine majirani zao wakizungumza.

“Ati naye huyo Zena anajitia mwanjani, ataka ubunge,” mmoja alianza.

“Ha! Hawakupata wanaume wa kweli atapata yeye mzio?” Mwengine akajibu.

“Na watakaompa yeye wamekosa kazi! Hebu yeye aweza kufanyani? Wanaume hawakuweza kufanya lolote ataweza yeye?” wa tatu akaendeleza mjadala.

Mmoja wao aliyekuwa karibu na aliyekuwa akiwasikiliza kwa kituo akavuta kauli na kusema, “Si basi mujaribu mumpe. Asaa kunfa yakuni yeye atawafanyia muyatakayo.”

“Bure yako,” akajibisha kwa ukali. “Kipande changu nitakiuza nijipatie gora ya leso na shilingi mia mbili. Niipoteze bure nikijua naisoza?” aliendelea.

Rayya Timamy, *Uteuzi wa Moyoni* (2004)

(a) Jadili ni kwa njia gani na kwa athari gani mwandishi ametumia mbinu za kifasihi kukuza dhamira kuu ya kifungu hiki.

(b) Toa maoni kuhusu mbinu zilizotumika kukuza wahusika katika kifungu hiki na jinsi mbinu hizi zinavyochangia kuwasilisha maudhui.

**2.**

**Kifungo**

Mtu kupata ajali, kawaida ya maisha,
Neno hili la ukweli, wahenga walifundisha,
Hakuna mtu kamili, dunia isomwangusha,
Hata likiwa jabali, watu wasilotingisha,
Litafika jembe kali, siku kulisimamisha,
Mtu kamwe sikejeli, kifungo atakipisha,
Usiku wetu wa kiza, uko katika kifungo.

Dunia ni kama wavu, majini unotembea,
Na ndoana yenye nguvu, watu inayowavua,
Si sisimizi na ndovu, itakapowatatua,
Na wawe na lovulovu, nguvu za kuizuwia,
Haishi watoa povu, kila inapoamua,
Dunia huvunja mbavu, bila kuitegemea,
Ulimwengu unacheza, na watu kwenye kifungo.

Katika chuo cha dhiki, kipindishacho migongo,
Unapochomwa mkuki, kikakufika kifungo,
Ikiwa hauna haki, usikiweke kinyongo,
Bali vumilia siki, izidi kula ubongo,
Wakati ukitaliki, ndio wa kuzaa tungo,
Mtu kukwaa kisiki, siyo kulamba udongo,
Wakati wa kujifunza, uko katika kifungo.

Maji huunguza sana, yanapotoka jikoni,
Na nyoka naye hutuna, akichokozwa mwilini,
Muda wa mwali kunena, akishatoka jandoni,
Mauti huacha jina, atokapo mazikoni,
Kila aliapo mwana, hunena kitu kinywani,
Kilicho bora hufana, ghamidha ikiauni,
Kariha ya miujiza, mzaziwe ni kifungo.

Charles Mloka, *Diwani ya Mloka* (2002)

(a) Jadili matumizi ya jazanda na mchango wake kimaana katika shairi hili.

(b) Unaweza ukasema nini kuhusu vile mshairi ametumia toni na sauti kumshawishi msomaji umuhimu wa dhamira ya shairi hili?